


## MAADILI YA MSINGI

Wakala utafanya kazi na kujipambanua kwa maadili ya msingi yafuatayo:

- (i) Uadilifu: Kufanya kazi kwa uaminifu na ukweli kwa wateja na wadau mbalimbali.
- (ii) Utendaji: Kazi wa Pamoja Kufanya kazi kwa pamoja na kushirikiana miongoni wa watumishi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.
- (iii) Utaalamu: Kuhakikisha tunazingatia utaalamu na kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu.
- (iv) Uwajibikaji: Kujituma katika utendaji kazi na kutimiza matakwa ya wadau na taifa kwa ujumla.
- (v) Uwazi: Kufanya kazi kwa uwazi na kuwa tayari kukaguliwa katika masuala ya kifedha na kiutendaji.



### Kwa maelezo zaidi wasiliana:

Mtendaji Mkuu  
Wakala wa Ufundi na Umeme  
(TEMESA)  
Keko Mwanga Industrial Area  
(Off Nyerere Road)  
S.L.P. 70704  
DAR ES SALAAM



022 2862796



temesatanzania

[info@temesa.go.tz](mailto:info@temesa.go.tz)

[www.temesa.go.tz](http://www.temesa.go.tz)



**JAMHURI YA MUUNGANO  
WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI,  
UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
WAKALA WA UFUNDI NA UMEME  
(TEMESA)**

## UTANGULIZI

Wakala wa Ufundi na Umeme (The Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (TEMESA)) ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya mwaka 1997 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 254 la tarehe 26 Agosti, 2005. Wakala ulizinduliwa rasmi na Serikali tarehe 23 Juni, 2006.

Lengo kuu la uanzishwaji wa TEMESA, ni kutoa kwa ufanisi huduma za kihandisi kwa Serikali, Taasisi za Umma na watu binafsi katika nyanja za uhandisi wa mitambo, umeme na elektroniki.

## DIRA

Kuwa Taasisi yenye ufanisi na bunifu inayotoa huduma za kihandisi Tanzania bara kwa ajili ya kumridhisha mteja ifikapo 2021.

## DHIMA

Kutoa huduma za uhakika, salama na zenye ubora wa hali ya juu katika

fani ya uhandisi mitambo, umeme na elektroniki, huduma za vivuko na ukodishaji mitambo kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

## MAJUKUMU YA WAKALA

Majukumu ya msingi ya Wakala ni kama ifuatavyo:

- (i) Kufanya matengenezo ya Magari, pikipiki na Mitambo ya Serikali katika Karakana ambazo zipo kila Mkoa;
- (ii) Kufanya matengenezo na Usimikaji wa Mifumo ya Umeme, Mabarafu, viyoyози na Elektroniki;
- (iii) Kufanya matengenezo ya taa za kuongozea magari (Traffic Signals) na taa za barabarani (Street Lights);
- (iv) Kukodisha magari kwa ajili ya usafiri wa Viongozi (VIP Vehicles) yaliyopo katika Kitengo cha GTA (Government Transport Agency) ;

(v) Kukodisha mitambo ya kuzalisha kokoto, na mitambo ya kazi za barabara;

(vi) Uendeshaji wa Vivuko vya Serikali;

(vii) Kutoa ushauri wa Kitaalamu kwa Serikali na Umma kwa ujumla katika nyanja za uhandisi wa Ufundi, Umeme na Elektroniki;

(viii) Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu usimikaji wa mifumo mipya ya uhandisi wa Ufundi, Umeme na Elektroniki; na

(ix) Kufanya usanifu na Usimamizi wa usimikaji wa mifumo ya uhandisi wa Ufundi Umeme na Elektroniki ili kukidhi viwango vinavyotakiwa na kwa kulingana na matakwa ya Sheria na Taratibu zinazoongoza taaluma husika.